

HOTUBA YA UFUNGUZI YA MGENI RASMI WAKATI WA UFUNGUZI WA KIKAO CHA WADAU WA UVUVI KANDA YA ZIWA TANGANYIKA KINACHOFANYIKA WILAYA YA SUMBAWANGA MKOANI RUKWA.

- *Kamishna wa Operesheni na Mafunzo Jeshi la Polisi Tanzania*
- *Chief wa Operesheni na Mafunzo,*
- *Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma,*
- *Kamanda wa Kikosi cha Wanamaji,*
- *Wahe. Wakuu wa Wilaya,*
- *Wakurugenzi wa Halmashauri,*
- *Maafisa Uvubi kutoka Rukwa, Kigoma na Katavi,*
- *Wadau wa uvubi wa Ziwa Tanganyika na Rukwa,*
- *Wahe. Madiwani,*
- *Wenyeviti wa Vijiji,*
- *Watendaji wa Kata na Vijiji*
- *Wageni Waalikwa,*
- *Waandishi wa Habari,*
- *Mabibi na Mabwana.*

*Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....*

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii adhimu kumshukuru mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha sisi sote kukutana mahali hapa tukiwa wazima na wenyе Afya njema. Kipekee niwakaribishe wageni wote walio toka nje ya Mkoa wetu. Niwaambie tu kuwa Rukwa ni salama na ya kupendeza. Kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu salama na kulinda amani na utulivu wa nchi yetu. Pia niwapongeze Makamanda wote mliopo hapa kwa kuendelea kulinda amani na utulivu kwenye Maeneo yenu mnayoyaongoza.

**Ndugu Washiriki**, Usalama katika Maziwa yetu ya Tanganyika na Rukwa ni muhimu sana kwa maendeleo ya Kiuchumi ya Wananchi wetu hasa Wavuvi. Wavuvi katika maziwa hayo wamekuwa wakiwekeza fedha zao ili waweze kuvua na hatimae kjiongezea kipato chao kwa manufaa ya Familia zao na Nchi kwa ujumla. Hivyo Kikao cha leo nimeambiwa ni kwaajili ya kufanya tathimini ya hali ya usalama ndani ya ziwa Tanganyika na Rukwa. Hili ni suala muhimu sana kwa Maslahi ya Wananchi wetu wa Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma. Tume kuwa tukishuhudia baadhi ya Wavuvi kuporwa mali zao za uvuvi na Majambazi na hasa ziwa Tanganyika. Majambazi hawa huwa wanapora hasa vinapokaribia vipindi furani. Ni vizuri tukajidhatiti katika kulinda

usalama wa raia wetu na Wavuvi wetu wa ziwa Tanganyika na ziwa Rukwa.

**Ndugu Washiriki**, Kikao hiki pia kinalengo la kuhakikisha kuwa mnaona changamoto zilizopo za Kiusalama katika Ziwa Tanganyika na kuzifanyia kazi. Ni imani yangu kuwa Wadau wote waliopo hapa leo watatoa ushirikiano wa kutosha ili kujua kuwa tuna changamoto gani za kiusalama kwenye maziwa haya ili serikali na Jeshi la Polisi waweze kuzifanyia kazi.

**Ndugu Washiriki**, Kikao hiki pia nimeambiwa mtajadili masuala ya uvuvi haramu, uhamiaji haramu na uporaji, Agenda hii ni muhimu sana ukizingatia kuwa kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na changamoto ya uvuvi haramu katika maziwa yetu ya Tanganyika na Rukwa. Hali hii inasababisha rasilimali za uvuvi kupotea na hati maye kipato cha Wananchi kushuka hasa Wavuvi. Ni vizuri kikao hiki kije na maazimio ya namna gani tunaweza kukabiliana na changamoto ya uvuvi haramu ambayo wakati mwingine baadhi ya maafisa uvuvi wetu wasiokuwa waaminifu nao wanachangia kwa kiasi kikubwa kwa kuendekeza masuala ya rushwa kwa wavuvi haramu.

**Ndugu Washiriki**, Ninafahamu kuwa mwezi machi, 2023 huko katavi kilifanyika kikao kama hiki ambapo mliweka maazimio matano. Ni imani yangu kuwa katika kikao hiki cha leo mtajadili ni

namna gani mmetekeleza maazimio hayo matano mliyoyaweka na wapi hamkutekeleza ili muweke msukumo zaidi. Vikao hivi vya kiutendaji ni vizuri sana kwani vinaisaidia serikali kujipanga vizuri katika masuala ya kiusalama na namna ya kukabiliana na uvuvi haramu katika ziwa Tanganyika na Rukwa.

**Mwisho**, Nawaomba washiriki wote mlionhuduria katika kikao hiki muwe na mijadala ya kina itakayosaidia kuleta mabadiliko makubwa ya usalama wa ziwa Tanganyika na ziwa Rukwa na hatimaye kusaidia Wananchi wetu kuishi kwa amani. Kama kuna changamoto zinazohusu Maafisa wetu wa Serikali wasio waadilifu pia mtuambie ili baada ya kikao hiki tuonyane na kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu mpandwa Dkt Samia Suluhu Hassan kutekeleza majukumu ya kuhakikisha kuwa Wananchi wake wanakuwa salama.

Mungu Ibariki Tanzania,

Mungu Bariki Mkoa wa Rukwa,

Asanteni kwa kunisikiliza

Charles Makongoro Nyerere

**Mkuu wa Mkoa wa Rukwa**